*Hii ni tafsiri isiyo rasmi ya toleo la Kiingereza, ambalo lililochapishwa na CHS Alliance. Chapisho hili lilitafsiriwa kwa uhuru na mashirika yafuatayo: Social Development Direct na Shirika la Translators without Borders. Timu ya CHS Alliance haihusiki na ubora na usahihi wa tafsiri hii.*

# MAREKEBISHO YA KIELEZO CHA CHS CHA ULINZI DHIDI YA UNYONYAJI, DHULUMA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA (OKTOBA 2020)

| Kiashiria cha CHS | Mahitaji ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia (PSEAH) | Maswali ya Kuongoza ya PSEAH | Ushahidi unaopendekezwa |
|---|---|---|---|
| **Ahadi ya 1: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanapokea msaada unaofaa na kuambatana na mahitaji yao.** | | | |
| 1.2 Programu zimebuniwa na kutekelezwa ipasavyo kulingana na tathmini isiyo na upendeleo ya mahitaji na hatari na ufahamu wa udhaifu na uwezo wa makundi tofauti. | Programu zinahitaji kubuniwa na kutekelezwa kulingana na tathmini ya hatari za Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia (SEAH) na uelewa wa hatari za SEAH wa makundi tofauti. | • Hatari zinazohusiana na SEAH za makundi tofauti zimetambuliwa na kuchanganuliwa?<br>• Hatari zinazohusiana SEAH zinatambuliwa na kuchanganuliwaje?<br>• Muundo na utekelezaji wa programu unatathminiwaje na kubadilishwa ili kupunguza hatari za SEAH na kuhakikisha hatari za SEAH hazijabuniwa au kuzidishwa? | • Muktadha, wadau na uchanganuzi wa hatari.<br>• Tathmini ya hatari ya SEAH - ama kama tathmini ya pekee ya hatari SEAH au kama kujumuisha SEAH katika tathmini pana ya hatari.<br>• Utaratibu na zana zinazohusiana kuhakikisha miundo ya programu inashughulikia udhaifu na hatari SEAH. Hii inaweza kujumuisha kiolezo sawazishi cha muundo wa programu ambacho kinajumuisha hiki kama sehemu inayohitajika, na/au kiolezo cha tathmini ya muundo wa programu ambacho kinajumuisha hiki kama kigezo kinachohitajika. |
| **Ahadi ya 2: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanafikia misaada ya kibinadamu wanayohitaji kwa wakati sahihi.** | | | |
| 2.1 Programu zimebuniwa kwa kuzingatia vizuizi ili hatua inayopendekezwa iwe halisi na salama kwa jamii. | Programu zinahitaji kuzingatia vikwazo vya shirika na muktadha ili hatua inayopendekezwa iwe salama kuhusiana na PSEAH kwa jamii. | • Vikwazo vya shirika na muktadha vinavyohusiana na PSEAH vinatambuliwa na kuchanganuliwaje?<br>• Muundo wa programu umehawilishwaje ili kulinda usalama wa watu walioathirika na SEAH? | • Tathmini ya hatari ya SEAH - ama kama tathmini ya pekee ya hatari SEAH au kama kujumuisha SEAH katika tathmini pana ya hatari.<br>• Utaratibu na zana zinazohusiana kuhakikisha miundo ya programu inakabili hatari za SEAH. Hii inaweza kujumuisha kiolezo sawazishi cha muundo wa programu ambacho kinajumuisha hiki kama sehemu inayohitajika, na/au kiolezo cha tathmini ya muundo wa programu ambacho kinajumuisha hatari za SEAH) kama kigezo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kinachohitajika. |

| Ahadi ya 3: Jamii na watu walioathiriwa na janga hawaathiriwi vibaya na wamejitayarisha zaidi, wanastahimili na wana hatari kidogo kwa sababu ya hatua za kibinadamu. | | | |
|---|---|---|---|
| 3.6 Programu zinatambua na kuchukua hatua kwa athari mbaya au zisizotarajiwa kwa wakati unaofaa na kwa namna ya kimfumo, ikijumuisha katika maeneo ya usalama wa watu, usalama, utu na haki, unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia na wafanyakazi, utamaduni, jinsia, uhusiano wa kijamii na kisiasa, njia za kutafuta riziki, uchumi wa ndani, na mazingira. | Programu zinahitaji kutambua na kuchukua hatua juu ya athari hasi zisizotarajiwa zinazohusiana na SEAH. | • Tathmini ya mradi, muktadha na uchanganuzi wa wadau inajumuisha hatari zinazoweza kutokea za SEAH?<br>• Unaendeleaje kufuatilia na kutambua athari hasi au zisizotarajiwa za SEAH?<br>• Ikiwa athari mbaya zinazohusiana na SEAH zinatambuliwa, zinafanywaje kwa wakati unaofaa na kwa utaratibu? kama vile<br>  ○ Unawezaje kuhawilisha muundo wa programu?<br>  ○ Unatoaje msaada kwa manusura/wahasiriwa wa SEAH?<br>  ○ Je, wewe hushughulika kivipi pale mfanyakazi mwenza ndiye mhalifu? | • Ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara za hatari - kama mkakati wa kutambua, kutathmini na kupunguza uwezekano wa SEAH kila wakati.<br>• Sera ya Kufichua Uhalifu - kama mkakati wa kugundua uhalisi na uwezekano wa SEAH.<br>• Waratibu wa PSEAH - kama mkakati wa kufuatilia na kukabiliana na hatari na visa vya SEAH.<br>• Kuinua uelewa kuhusu SEAH miongoni mwa watu walioathirika - kama njia ya kuzua SEAH.<br>• Mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu PSEAH - kama njia ya kuzuia SEAH. |
| 3.7 Sera, mikakati na mwongozo vimebuniwa kuzuia programu kuwa na athari mbaya kama vile, kwa mfano, unyonyaji, unyanyasaji au ubaguzi wa wafanyakazi dhidi ya jamii na watu walioathiriwa na janga, na kuimarisha uwezo wa wenyeji. | Shirika linahitaji kuwa na sera, mikakati na mwongozo katika kimaandishi ili kuzuia SEAH. | • Una sera ambayo inashughulikia PSEAH?<br>• Una mwongozo katika maandishi na mpango wa kazi ili kusaidia utekelezaji wa sera hii?<br>• Una mikakati ya kuzuia na kuangazia SEAH ikijumuisha Kanuni za Maadili, kampeni za habari, mikakati ya malalamishi, na sera ya kufichua uhalifu?<br>• Utekelezaji wa sera na mpango wa kazi unafuatiliwa unatathniwa namna gani?<br>• Unayo Sera ya Kulinda Usalama Mtandaoni? (kwa mashirika ambayo yanaingiliana na watu walioathiriwa mtandaoni, au kukutana mtandaoni (kwa mfano kuunga mkono wanaharakati vijana kuunda makundi ya mitandao ya kijamii)? | • Sera ya PSEAH au ujumuishaji wa PSEAH katika sera pana ya kulinda usalama au iliyosawa nayo<br>• Mpango wa kazi wa utekelezaji wa PSEAH<br>• Sera ya kufichua uhalifu au kutolipiza kisasi (sera sawa na hiyo inayolinda wafanyakazi na wengine wanaofichua mwenendo mbaya kuhakikisha kutolipiza kisasi)<br>• Kanuni za Maadili<br>• Mkakati wa Malalamishi<br>• Tathmini ya Hatari ya SEAH<br>• Taratibu za Uchunguzi wa SEAH<br>• Msaada wa manusura/utoaji wa sera ya usaidizi/mwongozo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3.8 Mifumo iko kulinda usalama wa habari yoyote ya kibinafsi iliyokusanywa kutoka kwa jamii na watu walioathiriwa na janga linaloweza kuwaweka katika hatari. | Shirika linahitaji kuwa na mifumo ya kulinda usalama wa habari za kibinafsi zinazohusiana na visa vya SEAH inayoweza kuweka watu walioathirika katika hatari. | • Je, unayo sera na mwongozo wa kuhakikisha kulinda usalama wa habari nyeti ya kibinafsi inayohusiana na visa vya SEAH?<br>• Je, una mifumo gani kuhakikisha usalama wa habari nyeti ya kibinafsi inayohusiana na visa vya SEAH?<br>• Je, una mifumo gani kuhakikisha usimamizi uliokabidhiwa na mahitaji ya usiri kwa wafanyakazi wanaosimamia visa vya SEAH?<br>• Je, unayo sera au mwongozo ambao unahusiana na kukusanya habari za kibinafsi kwa madhumuni ya vifaa vya mawasiliano, utafiti na kadhalika ambayo inashughulikia:<br>  ○ idhini kwa ufahamu kwa matumizi ya picha na habari zilizokusanywa<br>  ○ mwongozo wa kujumuisha habari nyeti kama vile mtu binafsi ni manusura wa Ukatili wa Kijinsia (GBV) au SEAH. | • Sera ya Ulinzi wa Data<br>• Taratibu za ulinzi wa data kama vile makabati ya mafaili yanayofungwa, nenosiri linalolindwa na kukabidhiwa upatikanaji wa uhifadhi wa data za elektroniki.<br>• Mamlaka yaliyokabidhiwa ya kusimamia uchunguzi wa SEAH |
| **Ahadi ya 4: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanajua haki zao na stahiki zao, wanapata habari na kushiriki katika maamuzi yanayowaathiri** | | | |
| 4.1. Habari inatolewa kwa jamii na watu walioathiriwa na janga kuhusu shirika, kanuni linayozingatia, tabia zinazotarajiwa za wafanyakazi, na programu na matokeo yake. | Habari inayotolewa kwa jamii inahitaji kushughulikia masharti ya shirika na tabia inayotarajiwa ya wafanyakazi kuhusiana na PSEAH. | • Ni vipi habari kuhusu ahadi za shirika na tabia inayotarajiwa ya wafanyakazi inayohusiana na PSEAH huwasilishwa kwa watu walioathirika na kuwekwa hadharani?<br>• Je, hiyo inawezaje kuwekwa katika muktadha unaofaa na kushirikiwa kwa njia zinazopatikana na zinazofaa?<br>• Je, unafuatiliaje kwamba habari hii inaeleweka na watu walioathirika? | • Utaratibu ulio katika maandishi ambao unahakikisha utoaji wa habari kwa utaratibu na watu walioathiriwa kupitia majukwaa na njia mbalimbali ili kuhakikisha ufikiaji kwa wote.<br>• kanuni za maadili ambayo yanajumuisha tabia zinazotarajiwa za wafanyakazi.<br>• Mabango au brosha ambazo zinazowasilisha tabia zinazotarajiwa kwa watu walioathiriwa katika lugha na muundo unaofaa |
| 4.5. Sera za kushiriki habari ziko -na zinaendeleza desturi ya mawasiliano wazi. | Shirika linahitaji kuwa na sera ya kushiriki habari ambayo inashughulikia PSEAH. | • Sera yako ya kushiriki habari au mwongozo inashughulikiaje habari zinazohusiana na PSEAH?<br>• Je, utekelezaji wa sera hii unafuatiliwa na kutathminiwa vipi? | • Sera ya Kushiriki Habari au kisawe chake |
| **Ahadi ya 5: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanafikia mikakati salama na inayofaa kushughulikia malalamishi.** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5.1. Jamii na watu walioathiriwa na janga wanashauriwa kuhusu a. kubuni, b. utekelezaji, na c. ufuatiliaji wa michakato ya kushughulikia malalamishi. | Jamii na watu walioathirika wanahitaji kushauriwa kuhusu jinsi mchakato wa kushughulikia malalamishi utakavyojumuisha SEAH. | • Watu walioathirika wanashauriwaje katika muundo, utekelezaji na ufuatiliaji wa michakato ya kushughulikia malalamishi inayojumuisha kimahsusi ushughulikiaji wa ripoti za SEAH?<br>• Ni vipi upendeleo, hasa ule unaohusiana na upatikanaji, usalama na usiri, wa makundi tofauti huzingatiwa katika muundo wa michakato ya kushughulikia malalamishi ambayo kimahsusi hushughulikia ripoti za SEAH? | • Waraka wa mwongozo kuhusu kuanzisha mikakati ya malalamishi<br>• Ushahidi wa mashauriano na watu walioathirika.<br>• Mahojiano na wafanyakazi ambayo yanaonyesha wameshauriana na watu walioathiriwa<br>• Majadiliano na watu walioathiriwa ambayo yanaonyesha wameshauriwa na maoni yao yamejumuishwa katika muundo, utekelezaji na ufuatiliaji wa michakato ya kushughulikia malalamishi. |
| 5.2. Malalamishi yanakaribishwa na kukubalika, na inawasilishwa jinsi mkakati unaweza kupatikana na mawanda ya masuala unaoweza kuyashughulikia. | Mkakati wa kushughulikia malalamishi unahitaji kukaribisha na kukubali ripoti zinazohusiana na SEAH, na jamii zinahitaji kujua kinachoweza kuripotiwa na vipi. | • Je, unawezaje kuanzisha desturi ambapo malalamishi/ripoti za SEAH zinakaribishwa na kukubaliwa?<br>• Je, unaelezeaje jinsi malalamishi yanavyoweza kutolewa, kuhusu masuala yapi, jinsi majibu yanavyotolewa, wanachoweza kutarajia walalamishi wakati wa kutoa malalamishi na jinsi wanavyolindwa katika mchakato wote?<br>• Je, makala ya kuimarisha uelewa wa mikakati ya malalamishi kuhusiana na SEAH yamehawilishwa katika lugha za wenyeji na kufanywa kupatikana kwa makundi tofauti? | • Malalamishi yaliyoandikwa, ripoti na mfumo/utaratibu wa uchunguzi.<br>• Ushahidi wa mashauriano na watu walioathirika.<br>• Mabango/habari kuhusu mikakati ya malalamishi inaonekana katika maeneo ya umma ya jamii au maeneo ya mradi. |
| 5.3. Malalamishi yanashughulikiwa kwa wakati unaofaa, kwa haki na njia mwafaka. Mikakati ya kushughulikia malalamishi inaweka kipaumbele kwa usalama wa mlalamishi na wale walioathiriwa katika hatua zote. | Malalamishi au ripoti zinazohusiana na SEAH zinahitaji kushughulikiwa kwa wakati, kwa haki, mwafaka na njia salama. | • Je, mikakati yako ya kushughulikia malalamishi inawekaje/inaipaje kipaumbele usalama wa mlalamishi au mwathiriwa/mnusura na wale walioathiriwa katika hatua zote?<br>• Je, shirika lina mwongozo ulioandikwa wa utoaji wa msaada kwa manusura/msaada kwa mwathirika ambao unaojikita kwa mwathirika/manusura? Je, mwongozo huo umewekwaje katika muktadha wa nchi tofauti na katika ngazi zote za shirika (kwa mfano kutoka kiulimwengu hadi programu na nchini)?<br>• Je, muda gani uliowekwa wa kuchunguza na kutatua malalamishi/ripoti za SEAH, na muda huo umeandikwa?<br>• Je, malalamishi/ripoti za SEAH zinachunguzwa mara | • Sera, Taratibu na miongozo ya iliyoandikwa ya Kushughulikia Malalamishi inayozungumzia SEAH kimahsusi na kuainisha:<br>○ kupiga ripoti na mifumo/taratibu za uchunguzi ikiwemo muda uliowekwa<br>○ kujitolea kwa mtazamo unaojikita kwa mwathiriwa/manusura<br>○ taratibu za utoaji wa msaada / usaidizi kwa waathiriwa / manusura.<br>• Sera ya usaidizi wa Mwathiriwa / Manusura ambayo inazingatia wahanga / manusura, msingi wa haki, umri, ulemavu na unyeti wa kijinsia, usio na ubaguzi na unaofaa kitamaduni. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | moja na wafanyakazi wenye uweledi unaofaa katika kiwango sahihi cha mamlaka na utaalam (kwa mfano wachunguzi walio na mafunzo)? | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | • Je, mlalamishi au mwathiriwa/manusura anasaidiwaje na kupatiwa taarifa kamili (ndani ya vigezo vya usiri) wakati wote wa mchakato?<br>• Je, unajuaje ikiwa walalamishi na watumiaji wanaotarajiwa mikakati wanahisi malalamishi yao ya SEAH yamekuwa au yameshughulikiwa kwa njia ya haki, mwafaka na salama?<br>• Je, shirika lako linahakikishaje kuwa utekelezaji wa sera yake ya kutolipiza kisasi? | |
| 5.4. Mchakato wa kushughulikia malalamishi ya jamii na ya watu walioathiriwa na janga umeandikwa na upo. Mchakato huu unashughulikia programu, unyonyaji wa kijinsia na dhuluma, na matumizi mabaya mengine ya mamlaka. | Shirika linahitaji kuwa na mchakato ulioandikwa wa kushughulikia malalamishi na mchakato wa uchunguzi ambao unashughulikia SEAH, unaojikita kwa mwathirika/manusura, na kuweka majukumu ya lazima ya kupiga ripoti inayohusiana na SEAH. | • Je, sera yako ya Kushughulikia Malalamishi au mchakato ulioandikwa unashughulikiaje SEAH?<br>• Je, utaratibu wako ulioandikwa wa uchunguzi unashughulikiaje SEAH?<br>• Ni majukumu gani ya lazima ya kuripoti yanayohusiana na Unyonyaji wa Kijinsia, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia (SEAH) na haya yameandikwa wapi?<br>• Je, mchakato wa kushughulikia malalamishi unafuatiliwa na kukaguliwa mara kwa mara?<br>• Je, unahakikishaje kuwa shirika linaelewa na linatimiza majukumu yake ya lazima ya kupiga ripoti ya SEAH katika ofisi yake kuu na nchi zingine za utendaji ikijumuisha mahitaji ya kisheria, kiserikali na wafadhili na hatari katika muktadha tofauti? | • Sera iliyoandikwa ya kushughulikia Malalamishi, taratibu na miongozo inayozungumzia SEAH kimahususi na kujumuisha mchakato wa uchunguzi.<br>• Wachunguzi SEAH walio na mafunzo wapo kwa ajili ya shirika katika ngazi zote (kwa mfano wachunguzi wa ndani, mipangilio na mashirika mengine yanayofanya uchunguzi). |
| 5.5. Desturi ya shirika ambamo malalamishi yanachukuliwa kwa uzito na kushughulikiwa kulingana na sera na michakato iliyoainishwa imewekwa. | Shirika linahitaji kuwa na desturi ya shirika ambayo inachukua malalamishi ya SEAH kwa uzito na kuyashughulikia kulingana na Sera na michakato yake PSEAH. | • Je, uongozi katika shirika lako hufanya nini kuendeleza desturi ya shirika ambayo malalamishi ya SEAH inachukuliwa kwa uzito?<br>• Je, munaye mratibu wa Kulinda Usalama/PSEAH anayewajibikia utekelezaji wa sera na michakato ya PSEAH?<br>• Je, jukumu la PSEAH linatolewaje kwa muundo wa utawala wa shirika?<br>• Je, unayo lazima ya kupiga ripoti visa vya SEAH (habari ya siri ikiwa imeondolewa) kwa wasimamizi wakuu wa shirika na baraza linaloongoza kama inavyotakiwa kwa wafadhili na vyombo vya kisheria? | • Mratibu wa PSEAH<br>• Wachunguzi wa SEAH<br>• Mamlaka yaliyokabidhiwa kwa wajibu wa kusimamia visa vya SEAH<br>• Rekodi zinazoonyesha utatuzi wa visa vya SEAH<br>• Kuripoti tukio la Unyonyaji wa Kijinsia, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia (SEAH) kwa shirika hilo<br>baraza linaloongoza au kisawe chake<br>• Mabango/habari kuhusu mikakati ya malalamishi inayoonekana katika maeneo ya umma ya jamii au maeneo ya mradi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | • Je, malalamishi yaliyothibitishwa ya SEAH huchangia katika ama hatua za kinidhamu au athari za kimkataba kulingana na madai hayo?<br>• Je, mfumo wako wa usimamizi wa hatari za ngazi ya shirika unajumuisha hatari za SEAH?<br>• Je, ni sera gani au mwongozo ulioeleza majukumu ya wafanyakazi ya kupiga ripoti visa au tuhuma za SEAH au matumizi mabaya ya mamlaka na wengine, ikijumuisha wafanyakazi wenzao, wafanyakazi wa shirika lingine?<br>• Je, wafanyakazi (au vyombo vingine vya uchunguzi) wamechaguliwa, wamefundishwa na wamepewa rasilimali ili kuchunguza malalamishi ya SEAH kulingana na viwango vya kisheria, sheria za nchi na matendo bora? | |
| 5.6. Jamii na watu walioathiriwa na janga wanajua kamili tabia inayotarajiwa kwa wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu, ikiwemo ahadi za shirika zilizowekwa kuhusu kuzuia unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia. | Shirika linahitaji kuhakikisha kuwa watu walioathiriwa wanajua kamili tabia inayotarajiwa kwa wafanyakazi kuhusu PSEAH, na ahadi za shirika kuhusu PSEAH. | • Je, unahakikishaje wafanyakazi wanaweka ifaavyo habari katika muktadha na kuisambazia jamii, kuhusu viwango vinavyotarajiwa vya tabia ya wafanyakazi na ahadi zinazohusiana na PSEAH? Je munao mwongozo kuhusu hili?<br>• Je, unafuatiliaje na kutathmini kwamba watu walioathiriwa wanaelewa tabia zinazotarajiwa za wafanyakazi kuhusu PSEAH, na ahadi za shirika za PSEAH?<br>• Je, unahakikishaje watu walioathiriwa wanajua jinsi shirika litashughulikia habari nyeti, kudumisha usiri na kutoa msaada kwao kwa malalamishi SEAH? | • Ushahidi wa mashauriano na watu walioathirika.<br>• Mabango au habari inayoelezea tabia inayotarajiwa ya wafanyakazi na ahadi za shirika kwa PSEAH zinazoonekana katika maeneo ya umma ya jamii au maeneo ya mradi<br>• Mjadala na watu walioathiriwa unaoonyesha uelewa wao wa tabia inayotarajiwa ya wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu, ikijumuisha ahadi za shirika zilizowekwa kuhusu kuzuia unyonyaji wa kijinsia na dhuluma. |
| 5.7. Malalamishi yaliyo nje ya upeo wa shirika yanapatiwa rufaa kwa shirika lingine kwa njia inayolingana na matendo bora. | Shirika linahitaji kutoa rufaa malalamishi/ripoti za SEAH ambazo ziko nje ya upeo wa shirika kwa shirika linalohusika kwa njia inayolingana na matendo bora. | • Je, unao mfumo wa rufaa ulioandikwa wa malalamishi /kupiga ripoti za SEAH?<br>• Je, ni mashirika gani mengine muhimu na huduma unazotolea rufaa yaliyo salama na ya nafaa kwa wasifu tofauti wa waathiriwa manusura wa SEAH?<br>• Je, unayo sheria na michakato maalumu ya shirika na nchi ya kupiga ripoti kwa lazima ikijumuisha jinsi na wakati wafanyakazi wanapopaswa kuwasiliana na mamlaka zinazofaa katika visa vya vitendo vya uhalifu au pale ambapo sheria ya kimataifa imevunjwa, ikiwemo visa vya SEAH? | • Mfumo wa rufaa ulioandikwa<br>• Usambazaji wa mfumo wa rufaa kwa wafanyakazi husika<br>• Mahojiano na wafanyakazi ambayo yanaonyesha ujuzi wao wa mahitaji haya na ya mashirika na huduma zingine zinazohusika. |

| Ahadi ya 6: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanapokea misaada inayoratibiwa, ya ziada. | | | |
|---|---|---|---|
| 6.1 Wajibu, majukumu, uwezo na masilahi ya wadau tofauti kutambuliwa. | Wajibu, majukumu na uwezo wa washirika na wadau wengine kuzuia SEAH uinahitaji kutambuliwa. | • Je, uzingatiaji wa masharti au michakato ya utathmini wa uwezo wa washirika huchunguza mifumo na uwezo wa PSEAH wa washirika wako?<br>• Je, unahakikishaje kuwa shirika lako na mashirika washirika wanaelewa majukumu ya lazima ya kupiga ripoti SEAH, athari za kisheria na kimuktadha na hatari kwa nchi zote ambapo operesheni za kikazi zinaendelezwa ? | • Michakato ya uzingatiaji wa masharti na violezo ambavyo zinashughulikia SEAH<br>• Michakato ya tathmini ya uwezo wa washirika na violezo ambavyo vinashughulikia SEAH. |
| 6.4 Habari inashirikiwa na washirika, makundi ya uratibu na watendaji wengine husika kupitia njia sahihi za mawasiliano. | Habari inayohusiana na PSEAH inahitaji kushirikiwa na washirika, makundi ya uratibu na watendaji wengine husika. | • Je, unahakikishaje uratibu na ushiriki wa habari kuhusu PSEAH na washirika, makundi ya uratibu na watendaji wengine?<br>• Je, unaratibu katika uchunguzi wa pamoja na mifumo ya pamoja ya ngazi ya utekelezaji kuhusu PSEAH?<br>• Je, shirika lako linashiriki katika kubadilishana data zinazohusu mienendo mbaya kuhusu SEAH baina ya Asasi mbalimabli? | • Uanachama katika bodi za uratibu na ushirikiano unaohusiana na PSEAH au kulinda usalama.<br>• Kumbukumbu za mikutano ya uratibu. |
| 6.6 Kufanya kazi na washirika kunatawaliwa na makubaliano wazi na thabiti ambayo yanaheshimu wajibu wa kila mshirika, majukumu na uhuru, na hutambua vikwazo na masharti yao. | Shirika linahitaji kuwa na makubaliano wazi na thabiti na washirika wake haswa kushughulikia majukumu ya PSEAH. | • Je, unashughulikiaje majukumu ya PSEAH katika makubaliano yaliyoandikwa na washirika?<br>• Je, uzingatiaji wa masharti ya PSEA na washirika hufuatijiwaje? | • Kiolezo cha makubaliano ya washirika na/au mifano ya mikataba ya washirika iliyosainiwa. |

| Ahadi ya 8: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanapokea msaada wanaohitaji kutoka kwa wafanyakazi na wahudumu wa kujitolea wenye uwezo na wenye kusimamiwa vizuri | | | |
|---|---|---|---|
| 8.1 Wafanyakazi hufanya kazi kulingana na wajibu na maadili ya shirika na kwa malengo yaliyokubaliwa na viwango vya utendaji. | Uajiri, uchunguzi na michakato ya utendaji wa wafanyakazi inahitaji kuendeleza kulinda usalama dhidi ya SEAH | • Je, ni michakato gani ya ajira na uchunguzi kwa wafanyakazi na washauri unaoendeleza SEAH muliyonayo?<br>• Je, shirika lako linashiriki katika kubadilishana data za mwenendo mbaya baina ya Asasi mbalimbali?<br>• Je, utathmini wa utendaji wa wafanyakazi unajumuisha kufuata kanuni za maadili, kukamilisha mafunzo yanayotakikana na masharti ya PSEAH?<br>• Je, sera yako ya rasilimali watu na mikataba ya ajira inabainisha wazi hatua za kinidhamu na vifungu vya kukomesha ajira mwenendo mbaya wa wafanyakazi ikijumuisha SEAH?<br>• Je, shirika lako lina mifano ya kukomesha ajira kama hatua ya kushughulikia visa vilivyothibitishwa vya SEAH? | • Taratibu za kuajiri na uchunguzi zilizoandikwa zinazojumuisha:<br>○ Matangazo ya kazi yanayorejelea ahadi za shirika kuhusu PSEAH<br>○ Ukaguzi wa historia yoyote ya uhalifu kupitia polisi (inapowezekana na salama)<br>○ Ukaguzi wa data ya mwenendo mbaya kutoka kwa asasi mbalimbali, inapowezekana<br>○ Maswali ya mahojiano yaliyolengwa yanayohusiana na PSEAH<br>○ Ukaguzi ulioandikwa na wa maongezi wa marejeleo ikijumuisha maswali yaliyolengwa yanayohusiana na PSEAH.<br>• Sera ya Rasilimali Watu<br>• Mikataba ya Ajira |
| 8.2. Wafanyakazi wanafuata sera ambazo zinawafaa na wanaelewa athari za kutozifuata. | Wafanyakazi wanahitaji kufuata sera za PSEAH, ikiwemo wajibu wa lazima wa kupiga ripoti na kuelewa athari za kutozifuata. | • Je, unahakikishaje kuwa wafanyakazi wote katika ngazi tofauti na katika maeneo tofauti, wanapata mafunzo ya kuelekeza na ya ziada kuhusu sera za PSEAH na wajibu wa kupiga ripoti na athari za kutozifuata?<br>• Je, mikataba ya wafanyakazi inajumuisha marejeleo ya vikwazo kwa kutozifuata sera za PSEAH na kanuni za maadili? | • Mchakato wa kuanza kazi unaojumuisha maelekezo kwa sera ya PSEAH, sera ya kushughulikia malalamishi, sera ya kufichua uhalifu na kanuni za maadili na taratibu husika. |
| 8.7. Kanuni za maadili zipo ambazo zinaweka, kwa kiwango cha chini, wajibu wa wafanyakazi kutowanyonya, kutowadhulumu au vinginevyo kuwabagua watu. | Shirika linahitaji kuwa na kanuni za maadili zinazojumuisha uwajibikaji wa wafanyakazi na watu wanaohusika na mashirika, kutowanyonya watu kingono, kutowadhulumu au kutowanyanyasa na | • Je, mnazo kanuni za maadili zinazoeleza wajibu wa wafanyakazi na watu wanaohusika na mashirika, kutowanyonya watu kingono, kutowadhulumu au kutowanyanyasa na kufuata wajibu wa kupiga ripoti?<br>• Je, unahakikishaje wafanyakazi wanaelewa, wanasaini na kufuata kanuni za maadili? | • Je, kanuni za maadili zilizoandikwa zinazoshughulikia tabia zinazotarajiwa za wafanyakazi ikijumuisha na wajibu wa wafanyakazi kutowanyonya kingono au kutowadhulumu watu hadi wajibu wa kupiga ripoti. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kufuata wajibu wa kupiga ripoti. | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8.9. Sera zimewekwa kwa usalama na ustawi wa wafanyakazi. | Shirika linahitaji kuwa na sera za kulinda usalama wa wafanyakazi ili kuwalinda dhidi ya unyonyaji wa kingono, dhuluma na unyanyasaji, na kulipiza kisasi, ikiwemo sera ya Ulinzi wa Mfichua Uhalifu. | • Je, shirika lako lina sera ya usalama wa wafanyakazi ambayo inashughulikia hatari ya SEAH kwao?<br>• Je, shirika lako lina michakato iliyoandikwa ya uchunguzi wa unyonyaji wa kingono, dhuluma au unyanyasaji dhidi ya wafanyakazi?<br>• Je, shirika lako lina Sera ya Kufichua Uhalifu na inatekelezwaje?<br>• Je, shirika lako hufanya tathmini ya usalama kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira ya nje ya nchi inayojumuisha tathmini ya hatari ya SEAH? | • Sera ya Usalama wa Wafanyakazi<br>• Sera ya Unyanyasaji wa Kijinsia<br>• Mafunzo ya SEAH kwa wafanyakazi<br>• Sera ya Kufichua Uhalifu<br>• Tathmini za usalama kwa wafanyakazi |
| **Ahadi ya 9: Jamii na watu walioathiriwa na janga wanaweza kutarajia mashirika yanayowasaidia kusimamia rasilimali kwa ufanisi, kwa kufaa na kwa maadili.** | | | |
| 9.5. Hatari ya ufisadi imedhibitiwa, na hatua zinazofaa zinachukuliwa wakati visa vya ufisadi zinapotambuliwa. | Ukosefu mkubwa wa maadili unahitaji kuchukuliwa kwa uzito na kushughulikiwa. | • Je, uongozi katika shirika lako hufanya nini kuendeleza desturi ya shirika ambapo mwenendo mbaya huchukuliwa kwa uzito na kushughulikiwa? | |

Kwa habari zaidi kuhusu kiashiria cha PSEAH na jinsi kinavyotumika na mashirika yanayofanya uthibitishaji dhidi ya Kiwango Msingi cha Kibinadamu kuhusu Kiwango cha Ubora na Uwajibikaji (CHS), tafadhali rejelea Mfumo wa Uthibitishaji wa CHS Alliance hapa **https://www.chsalliance.org/get-support/resource/chs- verification-framework/**